

# Pata Chanjo Zako Zote Zinazohitajika za COVID-19

Oktoba 2023



TAARIFA

Chanjo za COVID-19 za 2023-2024 ambazo hutoa ulinzi dhidi ya aina za sasa zaidi za virusi zimeidhinishwa na zinapendekezwa kwa matumizi.

## Chanjo za COVID-19 za 2023-2024

- Kila mtu aliye na umri wa miezi 6 na zaidi anapaswa kupata angalau dozi moja ya chanjo mpya ya COVID-19 (Pfizer au Moderna) katika kipindi cha 2023-2024 ili aendelee kukingwa dhidi ya maradhi makali na kulazwa hospitalini.
- Kuchanjwa dhidi ya COVID-19 ndio njia salama zaidi ya kujenga kinga dhidi ya maradhi makali–hata kwa wale ambao waliwahi kupata COVID-19.
- Watu walio na umri wa miaka 5 na zaidi wanaweza kupata dozi moja ya chanjo ya COVID-19 ya 2023-2024 (Pfizer au Moderna) ikiwa angalau miezi miwili imepita tangu walipopata dozi yao ya mwisho ya chanjo yoyote ya COVID-19.
- Watu ambao wana mifumo dhaifu kwa wastani au sana ya kinga wanaweza kuhitaji dozi za ziada.
- Watoto walio na umri wa miezi 6 hadi miaka 4 wanaweza kuhitaji dozi za ziada kulingana na wakati na chanjo walizopata hapo awali za COVID-19.

## Pata Mahali pa Kuchanjwa Dhidi ya COVID-19

- Chanjo za COVID-19 za 2023-2024 zitapatikana katika vituo vya huduma ya msingi, famasia na ofisi za afya za eneo na mahali kwingine kote katika Vermont. Tafadhali wasiliana na kituo ambapo huwa unapata chanjo zako zingine za kawaida unapoweka miadi. Pata mahali pa kuchajwa katika [Vaccines.gov \(kiungo katika Kiingereza\)](#).
- Chanjo za COVID-19 bado zinatolewa bila malipo kwako, lakini kwa sasa zinalipiwa kama chanjo zingine. Kwa watu wengi, bima yao ya afya italipia gharama za kuchanjwa.
- Kwa watu ambao hawana bima ya afya, au walio na bima isiyolipia gharama za chanjo (nadra sana), [Mpango wa Chanjo wa Vermont \(kiungo katika Kiingereza\)](#) au [Mpango wa muda wa Bridge Access wa CDC \(kiungo katika Kiingereza\)](#) unaweza kulipia gharama.

- Mtu yeyote anaweza kuchanjwa katika Vermont, ikiwa ni pamoja na wale wanaoishi katika jimbo jingine, wasio raia wa Marekani au wasio na bima.

Kumbuka: Medicaid hailipii gharama za watoto walio na bima ya Medicaid ili kuchanjwa katika famasia za Vermont.

## Usaidizi wa Kupata Chanjo

- Mtu yeyote aliye na bima ya afya anaweza kuchanjwa ikiwa ataweka miadi katika [ofisi za afya za eneo \(kiungo katika Kiingereza\)](#). Ofisi za afya za eneo pia zinaweza kusaidia kuwachanja watu walio na chini ya umri wa miaka 65 ambao wana bima ya afya ikiwa wameshindwa kuchanjwa katika maeneo mengine kutokana na kukosa usafiri na vikwazo vingine.
- Unahitaji usaidizi wa usafiri? Ikiwa huna namna ya kusafiri kwenda kuchanjwa dhidi ya COVID-19, tafadhali wasiliana na mtoa huduma wa usafiri wa umma wa karibu au upigie [Muungano wa Usafiri wa Umma wa Vermont \(Vermont Public Transportation Association, VPTA\) \(kiungo katika Kiingereza\)](#) kupitia 833-387-7200.
- Wanafunzi wa lugha ya Kiingereza, au jamii ya wahamiaji au wakimbizi, ambao wangependa kupata maelezo zaidi wanaweza kuwasiliana na [Muungano wa Waafrika Wanaoishi katika Vermont \(Association of Africans Living in Vermont\) \(kiungo katika Kiingereza\)](#) (AALV) kupitia 802-985-3106.